



Miaka mingi iliyopita, Jua na  
Maji walikuwa marafiki.

Wote waliishi duniani.



Jua alipenda kumtembelea  
Maji mara kwa mara.

Lakini, Maji hakuwahi  
kwenda kumtembelea Jua.




Mwishowe, Jua alimwuliza Maji kwa nini hakuenda kumtembelea.

Maji alijibu kwamba Jua ana nyumba ndogo sana. Alisema, "Nikija na familia yangu, tutakutupa nje."



Maji alisema, "Ukitaka  
nikutembelee, jenga uwanja  
mkubwa. Watu wangu ni  
wengi mno. Wao  
huchukuwa nafasi kubwa."




Jua alirudi nyumbani kwa mkewe, Mwezi. Mwezi alimsalimu kwa tabasamu kubwa.

Kisha Jua akamwambia Mwezi kuhusu ahadi aliyompa Maji.



Siku iliyofuata, Jua alianza kuandaa uwanja mkubwa ambamo angemtumbuiza rafiki yake, Maji.



Uwanja ulipokuwa tayari,  
alimwalika Maji  
awatembelee.



Maji alipofika, alimwuliza  
Jua iwapo ingekuwa salama  
yeye kuingia ndani.


Jua alijibu, "Ndiyo, ingia  
rafiki yangu."






Maji akaanza kutiririka ndani ya nyumba!

Aliambatana na mamba, samaki, vyura, nyoka, konokono, na wanyama wote wa majini.




Muda mfupi baadaye, Maji alifika magotini. Alimwuliza Jua iwapo bado ilikuwa salama. “Ndiyo,” Jua alijibu tena.

Jamaa wengine wengi wa Maji wakaendelea kuingia.



Maji alifika kiwango cha upeo wa kichwa cha mtu. Alimwambia Jua, "Je, watu wangu zaidi wanaweza kuja?" Jua na Mwezi walijibu, "Ndiyo."

Maji alitiririka ndani zaidi hadi Jua na Mwezi wikalazimika kuning'inia kwenye paa.



Watu wa Maji waliendelea kuingia hadi wakafika juu ya paa la nyumba. Jua na Mwezi walilazimika kwenda juu angani.

Tangu wakati huo, Jua na Mwezi huishi angani.